Ecolebooks.com

***336/1***
***Lugha ya***
***Kiswahili***
***Paper 1***
***2:30Hours***

**ACEITEKA MOCK EXAMINATIONS 2019**

## Uganda Certificate of Education

**MITIHANI YA MWIGO**

LUGHA YA KISWAHILI 336/1

Karatasi ya Kwanza

**MUDA : SAA MBILI NA NUSU**

**MAAGIZO;**

- Jibu maswali **Manne tu.**
- Jibu maswali mawili kutoka sehemu **A** na mawili kutoka sehemu **B**.
- Swali la kwanza lina vipengele viwili. Chagua kipengele kimojawapo: **Ama (A) au (B).**
- Nadhifisha mwandiko wako.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON **ECOLEBOOKS.COM**

**SEHEMU A**

**AMA**

1. **(a) Andika insha isiyopungua maneno 300 wala kuzidi maneno 450 juu ya mojawapo ya mada zifuatazo :**

(i) Biashara nitakayofanya baada ya kuhitimu masomoni.

(ii) Muungano wa jumuiya ya Afrika mashariki una manufaa kuliko madhara. Jadili.

*(iii)* Tunga insha inayoishia na, *'.......tangu siku hiyo nilipata funzo kubwa maishani mwangu.'*

(iv) Kudra ya Mungu haikosi

**AU**

**(b) Andika insha mbili fupi kwa kuchagua mada mbili miongoni mwa hizi zinazofuata :**

(i) Wewe kama Afisa wa Mazingira Wilayani kwako. Andaa ripoti ambayo ungetolea wanakijiji ambao wamepatwa na shida ya ukame kwa ajili ya ukataji wa miti katika eneo lao. *(Tumia maneno 100- 180)*

(ii) Tangazo limechapishwa katika gazeti la *New vision* likitangaza nafasi ya kazi ya meneja wa kiwanda cha Mafuta. Mwandikie mkurugenzi wa kiwanda hicho ukiiomba nafasi ya kazi hiyo kupitia anwani S.L.P 256, Kampala. *(Tumia maneno 90- 120)*

(iii) Fikiria kama wewe ni katibu wa Kilabu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC Club) hapo shuleni kwako, andika kumbukumbu za mkutano wenu uliohusu mipango ya kuendeleza somo la Kiswahili shuleni. *(Tumia maneno 120- 160)*

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON **ECOLEBOOKS.COM**

(iv) Wewe ni kiranja mkuu wa shule yako na mwalimu mkuu amekwambia kutoa hotuba kwa wale wanafunzi waliotoroka hapo shuleni wakaenda diskoni usiku. Andika hotuba yako.

*(Tumia maneno 100- 200)*

2. *Soma taarifa ya habari ifuatayo kisha ujibu maswali yote yatakayofuata hapo chini yake;*

*(Alama 20)*

Hapo mwanzoni mwa dunia hii, Mwenyezi Mungu aliumba viumbe wengi sana duniani. Binadamu ndiye kiumbe aliyepewa uwezo na madaraka ya kuwa kiumbe mkuu wa viumbe wengine. Binadamu wa kwanza kuumbwa na Mungu ni Adamu na Hawa. Wanadamu hao Mungu aliwapa makazi mazuri katika shamba la Edeni. Mungu aliwaambia watengeneze familia yao kwa kuzaa watoto, waijaze dunia nzima. Mungu aliwawekea mwiko wa tunda. Waliambiwa kuwa wale matunda yote mengine pale shambani lakini wasile tunda haramu tunda kwa sababu kula tunda haramu ni dhambi kubwa. Hata ingawa Adamu na Hawa walionywa wasile lile tunda haramu, walilipuuza onyo la Mungu wakafanya makosa ya kula tunda haramu.

Mungu alikasilika sana na kuwafukuza moja kwa moja waovu hao watoke kwenye shamba lake tukufu na kuwatupa hapa duniani. Tangu siku hiyo, Mungu alimlaani binadamu. Bindamu ni kiumbe aliyelaaniwa. Hii ndiyo sababu mwanadamu anateseka kupata chakula na kila kitu. Kosa la Adamu na Hawa ni chanzo cha shida, changamoto na kuteseka kwa vizazi vinavyowandama. Mtu anaitwa binadamu au mwanadamu kwa sababu watu wote duniani vizazi vyote vinatokana na familia ya Adamu. Sisi sote ni bin au wana wa Adamu –wanadamu pengine binadamu. Maneno hayo yameandikwa katika Vitabu vitakatifu vya dini; Bibilia ya wakristo na Korani ya waislamu.

Kuna viumbe wa aina nyingi duniani. Kwa mfano; wanyama, ndege na wadudu. Kuna Wanyama wa aina mbili; wanyama-pori na wanyama wanaofugwa nyumbani. Wanyama-pori wanakaa kwenye mbuga za wanyama misituni/porini/mwituni na majini. Wanyama wanaokaa misituni au porini ni kama vile; Simba, chui, Tumbili, Kifaru, swala, Nyati, Tembo, kuchakuro, Twiga, Pundamilia, Fisi, Mbweha, nakadhalika. Kwa nchi kama Uganda wanyamapori wanasaidia nchi kuingiza pesa za kigeni kutoka kwa watalii kama wazungu wanakuja kutazama wanyamapori wetu waliyo kwenye mbuga za wanyama kama vile; Kidepo na Queen Elizabeth. Pia kuna wanyama pori wanaokaa majini kama; Samaki, Mamba na Kiboko.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON **ECOLEBOOKS.COM**

Kuna wanyama wanaofugwa nyumbani kwa binadamu. Miongoni mwa wanyama wanaofugwa ni; Ng'ombe, Mbuzi, Mbwa, kondoo, punda, Ngamia, Nguruwe, Sungura , paka, panya na farasi. Wanyama hawa ni muhimu sana. Wanyama wanaleta faida kubwa mno kwa binadamu. Kwa mfano; Wanyama wanatupatia nyama ambayo ni chakula kwa binadamu, Wakulima wanapata pesa nyingi baada ya kuuza wanyama sokoni, wanyama wanafanya kazi kubwa ya kusafirisha watu na kubeba mizigo mizito. Wanyama pia wanatupatia mazao mengi kama vile; siagi (mafuta) ya kukaangia chakula, maziwa ya kunywa kama chai, ngozi za wanyama zinatusaidia kutengenezea viatu, ngoma, mikoba, nguo, kofia, silaha miongoni mwa vitu vingine vingi sana. Wanyama pia wanafanya kazi ya kulinda usalama nyumbani kama askari nyumbani. kwa mfano mbwa, akimwona mtu mgeni au mwizi akiingia hapo nyumbani, mbwa ataanza kubweka bwe bwe bwe! na kumfukuzia mbali.

Ndege au nyuni ni wa aina mbili; kuna ndege pori na ndege wanaofugwa nyumbani. Ndege wanaokaa porini au mwituni ni kama; Mbuni, kanga, korongo, Tausi, Kwale, tai, kipanga, Bundi, Mwewe na kadhalika. Ndege wanaofugwa nyumbani ni kama vile; Kuku, Bata, Kasuku, Batamzinga na Njiwa. Umuhimu wa ndege kwa binadamu ni kama; Kupata nyama ambayo ni chakula kwa binadamu, Ndege wanapatia binadamu mayai ya kula, Binadamu anapata pesa nyingi baada ya kuuza mazao ya ndege kama vile, mayai na nyama ya ndege.

Viumbe wengine ni wadudu. Kuna wadudu wengi sana duniani kwa mfano; Mchwa, kumbikumbi, senene, panzi, kipepeo, kiwavi, siafu, sisimizi, kupe, funza, nyuki, Nzi, Mbu, Mende, mabuu, nakadhalika. Wadudu wana faida na *madhara chungu nzima*. Kwa upande wa mazuri, yaani faida za wadudu kwa binadamu ni kama vile; Nyuki wanatengeneza asali ambayo ni tamu sana kwa binadamu, Wadudu ni chakula kwa binadamu. Wanadamu wengi wanakula wadudu kama vile; Kumbikumbi, mchwa na Senene. Kwa upande wa uhatari au mambo mabaya ya wadudu, wadudu wanasababisha madhara makubwa kwa binadamu kwa mfano; wadudu wanasambaza ugonjwa kwa binadamu. Kwa mfano; Mbu wanasambaza ugonjwa wa malaria. Nzi wanasambaza ugonjwa wa kipindupindu na waba. Wadudu wengine wanasumbua sana mwanadamu wanang'ata, wanauma, wanawasha na kuleta maumivu makubwa kwa mwili wa binadamu. Wadudu pia husababisha madhara makubwa kama vile kuharibu mimea ya wakulima shambani. Wadudu wengi wakiwemo nzige na viwavi ni waharibifu wakubwa wa mimea hapa nchini.

***Maswali;***

a) Pendekeza mada mwafaka kwa habari hiyo. *(Alama 01)*

b) Mwenyezi Mungu aliumba binadamu gani kwanza na walipewa makazi wapi? *(Alama 02)*

c) Adamu na Hawa walifanya dhambi gani mpaka wakafukuzwa shambani Edeni? *(Alama 02)*

d) Wadudu wana madhara gani kwa watu kama wananchi wa Uganda? *(Alama 02)*

e) Ndege wana umuhimu gani kwa watu wa jamii au nchi yako? *(Alama 02)*

f) Andika umuhimu au faida tano za wanyama kwa Wananchi wa nchi yako. *(Alama 05)*

g) Wewe kama mwanafunzi unapata mafunzo gani kutoka kwenye hadithi hiyo? *(Alama 04)*

h) Toa maana ya vifungu vya maneno hivi kama vilivyotumika katika habari;

   i) Mbuga za wanyama. *(Alama 01)*

   ii) madhara chungu nzima. *(Alama 01*

## ***SEHEMU YA 'B'***

**3. Fupisha habari ifuatayo kwa maneno 80 ukizingatia *'Umuhimu wa muziki'*.** *(Alama 20)*

Mtu yeyote hapa duniani ana kitu anachokipenda zaidi ndani ya moyo wake. Mimi ninapenda muziki kwa moyo wangu wote. Watu wote wanaume kwa wanawake wanapenda muziki. Muziki ni burudani ya maana sana katika maisha ya mwanadamu. Kuna umuhimu mwingi wa muziki katika jamii yetu. Kwa mfano; Muziki huburudisha watu katika jamii – wanaimba na kucheza muziki kwa furaha kwenye matamasha na diskoni.

Muziki unapatia watu kazi au ajira na wanamuziki wanapata pesa nyingi kutokana na kazi yao ya kucheza na kuimba nyimbo. Pia muziki ni chanzo cha furaha na ni faraja kwa watu wenye shida, mawazo, huzuni na matatizo mengine ya dunia. Muziki pia ni chanzo cha mapato ya nchi. Nchi nyingi kama vile Jamaica wanaingiza pesa nyingi za kigeni kutokana na muziki wao. Muziki hufundisha tabia nzuri kwa watu katika jamii. Muziki hukuza na kusambaza lugha husika katika jamii; Kwa mfano Kiswahili kuna waimbaji au wanamuziki wanaoimba nyimbo zao kwa kutumia lugha yetu nzuri ya Kiswahili.

Pia muziki ni chanzo cha umaarufu au kujulikana kwa watu hawa wanamuziki katika jamii zetu. Waimbaji karibu wote tunapata kuwajua kupitia nyimbo zao wanazoimba. Kwa mfano hapa nchini Uganda kuna mtoto maarufu sana anaitwa Fresh Kid. Fresh Kid

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

ni mwimbaji mpya mwenye umri wa miaka Saba tu. Anaimba nyimbo za miondoko ya kisasa zenye mtindo wa Hip-hop. Dunia nzima imepata kumjua mvulana huyu Fresh Kid kwa sababu anaimba vizuri. Kwa hivyo, umaarufu wa Fresh Kid umetokana na muziki wake.

Watu wengi wanaenda kwenye matamasha, Kilabu na diskoni usiku kwa sababu wanataka kusikiliza na kucheza muziki mzuri wa waimbaji hao. Vijana wa siku hizi wavulana kwa wasichana wanajua kucheza muziki vizuri. Wasichana wanatingisha matiti na matako yao pamoja na sehemu nyingine za mwili. Wavulana wanarukaruka juu na chini huku wakichanganya miguu yao. Lakini kati ya wavulana na wasichana ni nani wanaojua kucheza vizuri zaidi? Muziki ni mzuri kwa kila mtu hata wakiwa watoto wadogo, vijana, wakubwa na wazee. Kwa kweli,Watu wote wanapenda muziki duniani. Wazee wengi wanataka sana kusikiliza muziki wa zamani, yaani ule muziki wa kipindi chao . Baadhi ya wazee wanapendelea sana muziki mwororo wenye mwendo wa polepole.

**4. Tafsiri kifungu cha habari hiki kwa Kiswahili sanifu;** *(Alama 20)*

Life in a dormitory is very interesting. once you are introduced to dorm life you will not want to leave yet before you are there you can even weep your eyes out not wanting to even hear the word ‘dormitory’. one who will complete school life without staying in dormitory ,at least for a term, shall have missed something great in life. A dormitory is a class outside class.
As tiny boy going to senior one, I was told I would join a boarding school. young and powerless before my parents, I could not resist the proposal but after a week my father and I set off for school. I was received well by teachers but all in my mind was about what was going to happen to me in that chamber of hell called Dormitory. Whoever I saw before me was good as a devil according to what they could refer to as ‘Dorm-culture’.

I don’t want to take you through what happened at the beginning and what followed nor do I want to tell you the usual happenings in there. One thing I want to mention to you is that given a chance don’t stay outside a dormitory.
In a dormitory you will leave with people of various characters, you will meet thieves, misers, the kind, those who wet their beds, and many other types of people. What is most interesting to me in dorm life was the experience the misers went through. This is even why I called a dorm ‘class outside class’. My immediate dorm-neighbour, *Kwagala Blessed* was a very good miser. Whatever he would get immediately found its way directly into his suitcase; even if it was soup. What a funny boy!

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON **ECOLEBOOKS.COM**

One evening boys decided to teach him a memorable lesson. He had received well-prepared soup from his step mother and as usual he kept his gold in the safe place. There after he set off for preps. The teachers' reached for his suitcase; turned it upside down; shook it thoroughly and placed it back. Remember he had books, clothes and everything in the metallic case. Just imagine the kind of appearance he got on his face by the time he opened 'the safe place'.

## 5. Sarufi na matumizi ya lugha. *(Alama 20)*

Jibu kulingana na maagizo ya kila swali.

I. *ziandike sentensi zifuatazo katika hali ya kukanusha;* ***(Alama 2)***

a) Nikifundishwa vizuri darasani , nitafaulu bila shaka.
b) Musa huenda msikitini kusali kila Ijumaa

II. *Ziweke sentensi zifuatazo katika wakati uliopita hali timilifu;* ***(Alama 2)***

a) Wanasiasa waongo wanastahili kunyimwa kura zetu.

b) Makosa ni yetu sisi wapiga kura tunapowachagua marubani vipofu kwendesha ndege kila uchaguzi ufikapo.

III. *Andika tarakimu kwa maneno;* ***(Alama 2)***

a) 16:45 *Hours*
b) 0.038%

IV. *Andika vinyume vya sentensi zifuatazo;* ***(Alama 2)***

a) Mama alipoingia na bakora, baba akakurupuka nje upesi.
b) Kitinda mimba katika familia yangu ni mtoto wa kike

V. *Tegua vitendawili vifuatavyo kwa kutoa jibu sahihi ;* ***(Alama 2)***

a) Binadamu anaishi ndani ya sanduku …………..
b) Babu yangu kajenga nyumba ya nguzo moja tu ……………..

VI. *Kamilisha Methali zinazofuata;* ***(Alama 2)***

a) Asiyesikia la mkuu …………...
b) ………………………. haisitiri matako.

VII. *Ziweke sentensi zifuatazo katika hali ya Usemi wa taarifa;* ***(Alama 2)***

a) "Mwizi! Mwizi! Mmkamateni jamani!", Muuzaduka alipaaza sauti.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON **ECOLEBOOKS.COM**

b)Hellen alisaili , "Je, Kisitu keshokutwa itakuwa siku kuu?"

VIII. *Ziandike sentensi hizi katika Wingi;* ***( Alama 2)***

a) Ua lili hili ndilo utakalochukua harusini.

*b)* Ufa uo huo ndio utakaozibwa na mwashi.

IX. *Ziandike upya sentensi zifutatazo ukitumie kirejeshi 'amba..' badala ya* ***O****'rejeshi;* ***(Alama 2)***

a) Kaburini humo ndimo wanamozikwa wafu au maiti.

b) Sentensi zitakazosahihishwa na mwalimu si sahihi.

X. *Ziweke sentensi zifuatazo Katika hali ya Kutend**wa; (Alama 2)***

*a)* Mkunga mzee alikuwa anamzalisha mama mjamzito.

*b)* Mfanyabiashara maarufu hununua bidhaa ghali ng'ambo.

*MWISHO*

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON **ECOLEBOOKS.COM**